Mashirikisho ya Korea Kaskazini: Uhusiano Wake na Silaha, na Shughuli za Kuvunja Vikwazo

Imetayarishwa na Kathrin Kranz

1. UTANGULIZI

Mashirikisho ni mashirika makubwa yanayoundwa kwa kuunganisha biashara anuwai zilizo kando.[1] Mashirikisho ya Korea Kaskazini yamepangwa na kufdhiliwa vizuri, na yana sifa ya utata zaidi kwenye mbinu zao za kukiuka vikwazo. Mashirikisho ni sehemu muhimu ya sera ya mambo ya nje ya Korea Kaskazini na pia ni mbinu ya kupata pesa taslimu. Serikali ya Korea Kaskazini imeunda na/au kuunga mkono ukuaji wa mashirikisho kwa lengo wazi la kujenga uhusiano na nchi zingine kupitia uuzaji wa bidhaa za Korea Kaskazini, zikiwemo silaha na bidhaa na mafunzo husika. Kwa upande mwingine, mashirikisho yameisaidia serikali ipate pesa taslimu na vipuri vinavyohitajika kwenye mradi wake wa usamabazaji wa nyuklia.

Kwa hivyo, kufanya biashara na Korea Kaskazini ni upanga unaokata kuwili. Kwa upande mmoja, kununua bidhaa na huduma za Korea Kaskazini kunatoa fursa inayohalisi na inayoaminika kwa nchi nyingi zinazostawi. Kwa upande mwingine, inahusisha hatari madhubuti za sifa kwa nchi, haswa kwenye sekta nyeti ya biashara ya bunduki na silaha za nyuklia. Kwa ajili mashirikisho ya Korea Kaskazini yanashirikiana na wahusika wengine wenye sifa mbaya za kimataifa, kama vile Irani, hatari za kuhusishwa na nchi kama hizi ni madhubuti. Kuna uwezekano mkubwa sana kuwa mashirikisho ya Korea Kaskazini yataendelea kuwepo. Kwa mfano, kwenye kongamano baina ya Korea Kaskazini na Marekani huko Hanoi mnamo Februari 2019, wanachama wakuu wa ziara ya Korea Kaskazini ilizuru shirikisho kubwa kabisa la Vietinamu, Vingroup. Kulingana na ripoti za vyombo vya habari, Korea Kaskazini ilikuwa inchunguza njia za kuboresha uchumi wake.[2] Kwa ajili mashirikisho ya Korea Kaskazini yanaendelea na shughuli zao, yatafanya bidii ili kutafuta njia za kulinda shughuli zao ili kukwepa vikwazo. Ufahamu bora wa mashirikisho ya Korea Kaskazini, huduma na bidhaa zao, haswa shughuli zao ng'ambo, kwa hivyo ni muhimu kwa nchi na kampuni

[1] "mashirikisho" *OED Mtandaoni*. Oxford University Press, Juni 2018

[2] Eric Talmadge "Kando ya Kongamano, Wananchi wa Korea Kaskazini wanachunguza Uchumi wa Vietinamu," *ABC News*, Februari 27, 2019

Rico Carisch
rico.carisch@comcapint.com
+1-610-390-9541

www.comcapint.com
110 West 94 Street – 2D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
loraine.rickard-martin@comcapint.com
+1-917-715-2142

ambazo zina uhusiano na Korea Kaskazini, na ambazo zinataka kutii hatua zote za vikwazo vya Umoja wa Mataifa.

2. MASHIRIKISHO YA KOREA KASKAZINI NA UHUSIANO NA SILAHA

Mashirikisho ya Korea Kaskazini yanafafanuliwa vizuri kama "ushirikiano wa umma na kibinafsi."[3] Chini ya sheria za Korea Kaskazini, serikali ndiyo mwendeshaji pekee wa kiuchumi na kwa jumla inamiliki kampuni zote. Ingawa mashirikisho mengi yanaendeshwa kibinafsi, na pia kwa kiasi fulani kwa kutegemea ufadhili binafsi kutoka mabwenyenye matajiri wa Korea Kaskazini,[4] mashirikishi yana uhusiano wa karibu na serikali na Chama cha Wafanyakazi cha Korea Kaskazini.[5] Umuhimu wa mashirikisho haya unaonekana kuwa unaendelea kukua, kwa sababu kumekuwa na mwelekeo hadi "uanuwaishaji na ushirikishaji" wa baadhi ya majina maarufu zaidi ya chapa ya Korea Kaskazini,[6] ambayo inathibitishwa na idadi inayozidi kuongezeka ya bidhaa zinazotengenezwa nchini Korea Kaskazini kwenye maduka nchini Korea Kaskazini.[7]

Kwa mfano, Naegohyang, shirika la Korea Kaskazini linalomilikiwa na Korea Kaskazini, limebadilika kuanzia kuuza sigara hadi kuuza bidhaa kama vile bidhaa za elektroniki, vyakula vilivyookwa, na vinywaji.[8] Kampuni zingine za Korea Kaskazini ambazo zinageuka kuwa mashirikisho ni Air Koryo (kampuni ya ndege, teksi, vituo vya gesi, vinywaji) na Kundi la Korea Kumgang (teksi, benki, uajenti wa nyumba).[9] Shughuli za mashirikisho ya ndani ya nchi yanaungwa mkono kupitia juhudi za mashirikisho ya Korea Kaskazini yaliyoko ng'ambo, ambazo kwenye muktadha huu zinawakilisha chanzo cha kipato cha ubadilishanaji fedha cha Korea Kaskazini na zinasaidia kupata bidhaa zinazohitajika kwenye uzalishaji wa bidha nchini.[10] Kwa kuzingatia asili pana na yenye kina ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa, shughuli za mashirikisho zina uwezekano

---

[3] The Economist "Kuanzia Ndege hadi Makereli. Mfululizo Mpya wa Mashirikisho Yanayosaidia Korea Kaskazini," Januari 25, 2018

[4] Ibid. The Economist, 2018

[5] Ruediger Frank "Sera ya Korea Kaskazini 2018 na Mbeleni: Mabadiliko Hayapingiki, Ukawiaji Unawezekana," *38 North*, Agosti 8, 2018

[6] Andray Abrahamian "Vikwazo na Utafutaji Soko wa Korea Kaskazini" Mafunzo kutoka Myanmari," *38 Kaskazini*, Februari 28, 2018

[7] Sue-Lin Wong, James Pearson "Imetengenezwa nchini Korea Kaskazini: Vikwazo Vikali Zaidi Vinavyokaribia, Bidhaa Zaidi za Kienyeji Madukanis," *Reuters*, Mei 8, 2017

[8] Tia Han "Naegohyang: kampuni ya Korea Kaskazini inafanya shughuli mpya," *NK News*, Julai 18, 2018

[9] Ibid. Frank, 2018

[10] Heesun Wee "Kim Jong Un anakwepa vikwazo na anafuata mkakati huu wa nishati ili kuidumisha Korea Kaskazini," *CNBC*, Aprili 11, 2019

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

mkubwa sana wa kuhusisha ukiukaji wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa, au kukaribia sehemu za kijivu za shughuli zinazohusu vikwazo.

Hii haswa ndiyo hali kwani mashirikisho ya Korea Kaskazini yenye shughuli ulimwenguni mara nyingi ndiyo ambayo yanahusishwa kwenye biashara ya silaha na bidhaa na huduma husika. Kwa ajili ya asili yao nyeti, shughuli zinazohusu biashara ya silaha na bidhaa na huduma husika zinasababisha gharama madhubuti za sifa kwa nchi zinazopatikana kuwa zinashirikiana na Korea Kaskazini. Ripoti ya Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa ya 2019 ilidokeza kuwa Korea Kaskazini "ilijaribu kufikisha bunduki ndogo na silaha hafifu na vifaa vingine vya kijeshi hdi kwa wanamgambo wa Huthi [wanaosaidiwa na Irani] nchini Yemeni, na pia hadi Libya na Sudani, kupitia wapatanishi wa nje, wakiwemo mlanguzi wa silaha wa Siria Hussein al-Ali".[11] Kulingana na ripoti, Korea Kaskazini pia imeshirikiana na Siria na Irani ili kuunda vituo nchini Siria ambavyo vilitumiwa kutengeneza silaha za kemikali, ambazo kuna uwezekano mkubwa sana kuwa zilitumiwa na watawala wa Siria dhidhi ya wananchi wa Siria.[12]

Unaofaa kudokezwa kimahususi ni uhusiano na Irani, ambayo imefafanuliwa kama mteja bora kabisa wa Korea Kaskazini. Kwenye vita vya Irani na Iraki pekee, Korea Kaskazini ili hamisha silaha, mafunzo, na usaidzi wa kijeshi wenye thamani ya bilioni $1 hadi Irani.[13] Hivi karibuni, nchi hizi zimeshirikiana kwenye miradi yao ya nyuklia. KOMID imehamisha vijenzi na teknolojia za makombora ya mbali zilizovumbuliwa nchini Korea Kaskazini hadi kwa washiriki wao nchini Irani. Mashirikisho ya Korea Kaskazini ya KOMID/Green Pine, yaliyoorodheshwa yawekewe vikwazo na Umoja wa Mataifa yana ofisi nchini Irani.[14] Green Pine, pamoja na usaidizi wa wakala ya upelelezi ya Korea Kaskazini, Ofisi ya Jumla ya Upelelezi, pia imehusishwa na usafirishaji haramu wa silaha kutoka na kuelekea nchini Irani. Kwa upande mwingine, kuwepo kwa mashirikisho ya KOMID/Green Pine nchini Irani kumesaidia shughuli za mataifa mengine, ikiwemo barani Afrika.

Uhusiano wa Korea Kaskazini na nchi barani Afrika mara nyingi huwa unajumuisha ushirikiano wa kijeshi na/au unaohusu silaha na pia huduma za ujenzi. Kwa mfano, imedaiwa kuwa kituo cha kuzalisha na kukarabati silaha huko Nakasongola, Uganda, ambacho hapo awali kilipewa usaidizi na Uchina kilipoanzishwa, kimeungwa mkono na Korea Kaskazini.[15] Kwenye miaka ya hivi karibuni, uhusiano baina ya Uganda na Korea Kaskazini inaonekana kuwa ilikuwa inahusisha mafunzo na taaluma kwa vikosi vya usalama wa ndani vya Uganda na ufikishaji wa vifaa "visivyohatarisha".[16] Uhusiano umehusisha shirikisho la Korea Kaskazini, KOMID (shirikisho liloorodheshwa na Korea

[11] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, S/2019/171, muhtasari

[12] Nate Thayer "Miradi ya makombora na kemikali ya Siria na Korea Kaskazini," *Habari za NK,* 19 Juni 2013

[13] Bruce E. Bechtol Jr. "Biashara Haramu ya Silaha ya Korea Kaskazini," *Foreign Affairs*, 6 Juni 2018

[14] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 72

[15] "Madai kuwa Kampala imeongeza uwezo wa kutengeneza silaha," *The New Humanitarian*, 30 Machi 1999

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Kaskazini) na kwa upande mwingine, ushirikiano unaokaribia maeneo yasiyo wazi ya shughuli zinazohusu vikwazo.

3. MASHIRIKISHO

3.1 Shirika Husiani la Green Pine (Green Pine)/Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID)

Shirika Husiani la Green Pine (Green Pine) ilichukua nafasi ya Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID) baada ya KOMID kuorodheshwa mnamo 24 Aprili 2009. Green Pine ikaorodheshwa mbeleni mnamo 2 Mei 2012.[17] Green Pine/KOMID ndiyo mfanyabiashara mkuu wa silaha na muuzaji nje mkuu wa bidhaa na vifaa vinavyohusu makombora ya mbali na silaha za kawaida.[18] Inafanya shughuli chini ya uelekezi wa Ofisi ya Jumla ya Upelelezi, huduma ya kimsingi ya Korea Kaskazini ya upelelezi wa nje.[19]

Green Pine, na KOMID kabla yake, zinaendeshwa chini ya lakabu huko ng'ambi, na zinashirikiana na kampuni zingine ambazo zinaweza kuwa sehemu za mashirikisho yao moja kwa moja. Kwa kuzingatia utata wa mashirikisho ya Green Pine/KOMID na shughuli zao, ni muhimu kuzingatia baadhi ya mitandao iliyoanzishwa na Green Pine/KOMID.

Kwa mfano, KOMID ilishirikiana na Kundi la Kampuni la Miradi ya Nje ya Mansudae (Mansudae), kampuni ya ujenzi ya Korea Kaskazini. Mansudae imesimamia shughuli za ujenzi kwenye angalau nchi 14 barani Afrika, “kujenga kila kitu kuanzia mitambo ya silaha, ikulu za rais, hadi fleti za nyumba.”[20] Mansudae, hadi hivi karibuni, ilikuwa na makao makuu nchini Namibia, ambapo Mkurugenzi Msimamizi alikuwa Kim Tong Chol.[21] Iliorodheshwa mnamo 5 Agosti 2017 kwa kujihusisha kwenye, kurahisisha, au kuwasafirisha nje wafanyakazi kutoka Korea Kaskazini hadi kwenye nchi zingine, zikiwemo Aljeria, Angola, Botswana, Benin, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo,

---

[16] Andrea Berger “Kikomo cha Kisheria? Uhusiano wa Usalama baina ya Uganda na Korea Kaskazini,” *38 North*, 13 Novemba 2014

[17] Matawi Yanyomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kamati ya Baraza la Usalama Iliyoanzishwa kwa Kutii Azimio la 1718 (2006) “Shirika Husiani la Green Pine,” 2 Mei 2012

[18] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. “Orodha iliyoanzishwa na kudumishwa kwa kutii azimio la Baraza la Usalama la 1718 (2006). 24 Mei 2016

[19] UNSC, S/2012/422 (2012), Nyongeza X

[20] Hugh Griffiths alinukuliwa kwenye David McKenzie na Brent Swails “Masanamu na risasi: Uhusiano wa Korea Kaskazini barani Afrika,” *CNN*, 15 Disemba 2017

[21] Ibid. CNN, 2017; “Wizara ya Fedha Inalenga Watu Binafsi na Mashirika ya Uchina na Urusi Yanayounga Mkono Uongozi wa Korea Kaskazini,” Idara ya Marekani ya Kituo cha Uanahabari cha Wizara ya Fedha, 22 Agosti 2017

Ginekweta, Namibia, Togo na Zimbabwe.[22] Kwa pamoja, KOMID na Mansudae zilipatikana kuwa zimehusik kwenye ujenzi wa kiwanda cha silaha nchini Namibia.

Shirika la fedha la KOMID pia lilitegemea mashirika mengine, ambayo pia yalikuwa yametuhumiwa kwenye utekelezaji wa vikwazo. Banki ya Kibiashara ya Tanchon (iliyokuwa ikijulikana kama Benki ya Mikopo ya Changwang FKA: Benki ya Mikopo ya Korea Changwang) ilikuwa tawi kuu la fedha la KOMID.[23] Imehusishwa na idadi ya mashirika mengine yaliyoorodheshwa, yakiwemo Banki ya Maendeleo ya Amroggang na Shirika la Benki la Korea Kwangson Banking Corporation, ambayo pia inafanya miamala ya fedha kwa niaba ya KOMID.[24]

Green Pine, kwa wakati huo huo, inaendeshwa kwa kutumia lakabu anuwai, kama vile Shirika la Kuwekeza na Kuendeleza Rasilimali za Kiasili au Kampuni ya Madini Adimu ya Jumla.[25] Benki ya East Land ilirahisisha miamala inayohusisha silaha kwa, na ilitoa usaidizi mwingine kwa, Green Pine. Iliorodheshwa mnamo 29 Oktoba 2014 na "imefanya kazi kiamilifu na Green Pine ili kuhamisha fedha kwa njia inayokwepa vikwazo."[26] Rais wa Green Pine ni Ri Hak Chol, ambaye amesafiri hadi Angola, Misri, na Jamhuri ya Kiislamu ya Irani, licha ya vikwazo vinavyonuiwa kuzuia usafiri huu wa kimataifa.[27]

3.2 Glocom

Glocom ni mtandao wa kimataifa wa biashara unaoendeshwa na Ofisi ya Jumla ya Upelelezi ambao unauza teknolojia isiyoruhusiwa ya mawasiliano ya kijeshi na ina makao yake makuu nchini Malesia.[28] Inafanya shughuli kama kampuni inayoficha Pan Systems Pyongyang ya Korea Kaskazini, ambayo inafanya kazi muhimu ya kununua na kufadhili bidhaa nyeti zenye matumizi mawili kwa niaba ya Korea Kaskazini.[29] Glocom ina akaunti kadhaa huko kwenye nchi nne ambazo zimefunguliwa kupitia kampuni mbili

---

[22] "Baraza la Usalama Linongezea Nguvu Vikwazo Dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Korea, Kwa Pamoja Linaidhinisha Azimio la 2371 (2017)," *Matoleo ya Vyombo vya Habari na Kuangazia Mikutano ya Umoja wa Mataifa*, 5 Agosti 2017

[23] UNSC, S/2014/147 (2014), ukurasa wa 119

[24] Ibid. p. 121

[25] UNSC, S/2018/171 (2018), paragrafu ya 116

[26] Matawi Yanayomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kamati ya Baraza la Usalama Iliyoanzishwa kwa Kutii Azimio la 1718 (2006), Muhtasari Simulizi za Sababu za Kuorodheshwa, "Benki ya East Land," 29 Oktoba 2014

[27] UNSC S/2017/150 (2017), jedwali la 9

[28] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 173

[29] Scott A. Snyder "Shughuli Muhimu Iliyofanywa na Malesia Iliyowezesha Korea Kaskazini Ipate Silaha za Maangamizi Makubwa" *Baraza la Uhusiano wa Kimataifa*, Machi 6 2017

zifichazo zenye makao yake makuu nchini Malesia (Huduma za Kimataifa za Golden na Mfumo wa Kimataifa Ulimwenguni). Malipo ya Glocom kwa wafikishaji na uhamishaji kwenye mtandao yanahusisha kuhamisha fedha kutoka Korea Kaskazini, Uchina, Malesia, Singapoo, na Marekani, watu wa mpito, na kampuni ifichayo huko Hong Kong. Wapokeaji wanaona tu malipo kutoka kampuni ifichayo.[30] Hatua hizi za ulaghai na ukwepaji vikwazo zimeruhusu Glocom ishiriki kwenye biashara mashuhuri za uuzaji silaha kieneo na iuze silaha za daraja ya juu na nyenzo husika kwenye nchi kadhaa.[31] Kwa kweli, uwazi ambao imetumiwa kufanya shughuli zake ndiyo mojawapo ya sababu za kufaulu kwake: kutangaza bidhaa kwa uwazi kunaipatia Glocom kiwango cha uhalali.

4. Ukiukaji Muhimu wa Vikwazo Barani Afrika

Ukiukaji kadhaa wa vikwazo unaweza kurekodiwa kulingana na Umoja wa Mataifa na vyombo vya habari. Vikwazo anuwai, vikiwemo makatazo ya usafiri, na silaha, ushirikiano wa kijeshi, marufuku ya fedha na biashara, vimekwepwa.

4.1 KOMID/ Green Pine

4.1.1 KOMID

4.1.1.1 Namibia

KOMID ilitoa vijenzi muhimu vya ujenzi wa kiwanda cha silaha cha Oamites nchini Namibia kwa kushirikiana na, au kwa kutumia lakabu ya, Kundi la Kampuni la Miradi ya Nje ya Mansudae.[32] Mansudae ilitumia wafanyakazi kutoka Korea Kaskazini. Namibia ilithibitisha kuwa Mansudae ilihusika kwenye miradi kadhaa ya ujenzi wa kijeshi, ikiwemo chuo cha kijeshi na makao makuu ya Wizara ya Ulinzi, lakini ilikataa kuwa ilikuwa inajua uhusiano baina ya Mansudae na KOMID.[33]

Kwa ziada, KOMID ilifikisha aina kadhaa za matangi ya shinikizo na mashine nchini Namibia zinazoweza kutumiwa kwenye vilipuzi vya kijeshi na uzalishaji wa kemikali za urushaji.[34]

---

[30] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 176

[31] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 87

[32] UNSC, S/2016/157, paragrafu ya 101

[33] UNSC, S/2017/150, paragrafu za 103-104 na Nyongeza ya 70

[34] UNSC, S/2017/150, paragrafu za 110-112

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Ubalozi wa Korea Kaskazini nchini Korea Kaskazini uliwasaidia maafisa wa KOMID ambao kwa majina yao walifungua akaunti ya benki nchini Namibia.[35]

4.1.1.2 Uganda

Imeripotiwa kuwa KOMID ilitoa mafunzo kwa vikosi vya polisi na jeshi vya Uganda, na haswa vikosi vya wanahewa vya Uganda.[36] Shughuli hizi ziliungwa mkono na raia wa Korea Kaskazini na mtu binafsi aliyeorodheshwa, Ryu Jin. Alitumia Shirika la Biashara ya Teknolojia la Tosong na Banki ya Kibiashara ya Tanchon kama kampuni zinazomilikiwa ili kukwepa vikwazo alivyowekewa. Anaaminiwa kuwa anasafiri kwa kutumia lakabu.

Pia imeripotiwa kuwa ofisi ya mwakilishi wa jeshi kwenye Balozi ya Korea Kaskazini huko Kampala, Uganda, ilijaribu kutoa huduma za kijeshi zisizoruhusiwa.[37] Mnamo Disemba 2018, ripoti ya vyombo vya habari ilidai kuwa KOMID iliendelea na shughuli zake nchini Uganda, na kuwa ufikishaji wa silaha anuwai hadi nchini Uganda ulikamilishwa kwenye mwaka huo huo.[38] Ripoti ya Jopo la Wataalamu la 2019 lilidokeza kuwa huenda maafisa wa Uganda walikuwa wanajua kuhusu uhusiano na KOMID.[39] Pia imedokezwa kuwa miradi mengine ya pamoja isitoruhusiwa iliendelea kufanyika.

4.1.1.3 Sudani

Maafisa wawili wa KOMID nchini Sudani ni Kim Song Chol, ambaye pia anafanya shughuli kwa kutumia lakabu Kim Hak Song, na Song Jong Hyok, ambaye pia anatumia lakabu Son Min.[40] Maafisa wote wawili waliwahi kufukuzwa nchini Misri, na kulingana na ripoti, ni wahusika wakuu kwenye uhusiano baina ya Sudani na Korea Kaskazini. Inadaiwa kuwa KOMID inajihusisha na Shirika la Viwanda vya Kijeshi linaloendeshwa na Serikali ya Sudani. Kwa ziada, usafirishaji kadhaa angani na baharini kutoka Korea Kaskazini hadi nchini Sudani ambao unahusu KOMID unachunguzwa.[41]

---

[35] UNSC, S/2017/742, paragrafu ya 50

[36] UNSC, S/2017/742, paragrafu ya 29

[37] Ibid.

[38] Joe Parkinson "Usiwahi Kupiga Picha Zao: Kufuatilia Makomando, Uuzaji nje wa Siri wa Korea Kaskazini," *Wall Street Journal*, 10 Disemba 2018

[39] UNSC, S/2019/171, paragrafu za 93-94

[40] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa "Azimio la 2321 (2016). Lililoidhinishwa na Baraza la Usalama kwenye mkutano wake wa 7821, mnamo 30 Novemba 2016." Nyongeza ya Kwanza

[41] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 122

Korea Kaskazini pia ilifikisha vijenzi vya udhibiti wa roketi inayoelekezwa kwa

usahihi ya mm 122 na makombora themanini yanayoelekezwa na satalaiti ya kuvamia anga hadi kwa Kampuni Kuu ya Uhandisi wa Teknolojia ya Sudani. Mikataba ya mauzo hayo ilitiwa saini na rais wa KOMID Kang Myong Chol (lakabu yake ni Pak Han Se), kwa kutumia kampuni ifichayo ya KOMID Kampuni

Kuu ya Uhandisi wa Teknolojia ya Chosun.[42] Kim Song Chol, aliyekuwa anaishi Misri, alisafiri hadi Khartoum kama sehemu ya muamala huo, na aliandamana na wafanyakazi 13 wa KOMID.[43]

Kulingana na toleo la habari la Idara ya Marekani ya Fedha, mwakilishi wa KOMID Jang Song Chol, “anafanya kazi na watu nchini Sudani ambao wananunua nyenzo kwa niaba yake,” ambayo inazidi kuashiria miamala ya kijeshi baina ya Sudani na Korea Kaskazini.[44]

4.1.2 Green Pine

4.1.2.1 Angola

Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa lilichunguza wanadiplomasia wa Korea Kaskazini waliopewa vyeti nchini Angola waliokuwa wanafanya kazi kwa niaba ya Green Pine ambayo hapo awali imewahi kujihusisha kwenye shughuli zisizoruhusiwa zinazohusu silaha.[45]

Jopo pia linaendelea na uchunguzi kwenye mafunzo yaliyopewa walinzi wa rais wa Angola kutoka kwa wanadiplomasia na maafisa wa Korea Kaskazini waliopewa vyeti nchini Anglola na ambao wanafanya kazi kwa niaba ya Green Pine. Mwanadiplomasia moja, Kim Hyok Chan, alikuwa na jukumu la uundaji upya wa vyombo vya baharini vya Angola uliofanywa na Korea Kaskazini kwa ukiukaji wa vikwazo.[46] Yeye, pamoja na mwakilishi wa Green Pine, Jon Chol Yong, walisafiri hadi Sri Lanka mara tatu ili kuzungumzia miradi ya kujenga meli. Kulingana na Angola, Jon Chol Yong hayupo tena nchini Angola.[47]

---

[42] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 106

[43] Declan Walsh “Unahitaji Kombora la Korea Kaskazini? Pigia Simu Balozi ya Misri.” *The New York Times*, Machi 3, 2018 na UNSC S/2017/150, Jedwali la 3.

[44] Imenukuliwa kwenye Andrea Berger “Trump anaipatia Sudani (na ulimwengu) “onyo” kuhusu Korea Kaksazini” *Arms Control Wonk*, Julai 12, 2017

[45] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 85

[46] UNSC, S/2017/742, paragrafu ya 23

[47] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 62

Angola iliripoti kuwa Green Pine ilifikisha boti za kijeshi za kushika doria kwenye nchi hiyo hadi 2012. Rekodi za mamlaka za ushuru za Uchina pia zinaonyesha kuwa kampuni yenye makao yake makuu huko Beijing yenye uhusiano n Green Pine iliuzia Angola bidhaa zenye matumizi mawili za vyombo vya baharini, zikiwemo injini za boti, na mifumo ya rada. [48] Mnamo Februari na Julai 2011, raia wa Austria, Josef Schwartz aliisaidia Green Pine kusafirisha bidhaa za boti za kijeshi za kushika doria na vipuri vya nyambizi hadi nchini Angola.[49]

4.1.2.2 Misri

Shirika la Biashara la Saeng Pil, lakabu ya Green Pine, imekuwa ikifanya shughuli zake huko Kairo. Mwanadiplomasia wa Korea Kaskazini, An Jong Hyuk, aliteuliwa kama mwakilishi wa Shirika hilo, na mnamo 18 Disemba 2013, aliidhinishwa kufanya aina zote za shughuli za kibiashara, ikiwemo kufanya mikataba na kufanya biashara ya banki.[50] Imeripotiwa kuwa An Jong Hyuk alitoka Misri na hakurudi tena.[51]

4.1.2.3 Eritrea

Jopo la Wataalamu liliunga mkono uhusiano wa kijeshi baina ya Green Pine na Idara ya Magereji ya Serikali (ambayo ina jukumu la kudumisha na kuunda upya mifumo ya silaha).[52]

4.1.2.4 Libya

Juhudi kadhaa zimefanywa ili kuunda uhusiano wa kijeshi baina ya Korea Kaskazini na viongozi wa Libya ambazo zilihusisha Green Pine na zinachunguzwa na Jopo la Wataalamu.[53] Nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa anadai kuwa barua ya 2015 kutoka O Chol Su, DPRK Naibu wa Waziri wa Wizara ya Vifaa vya Kijeshi, hadi kwa Chifu wa Baraza Kuu la Ulinzi la Libya ilikuwa na maelezo kuhusu makubaliano ya ununuzi/uuzaji wa mifumo ya ulinzi na risasi. Green Pine, iliyofafanuliwa kama “shirika la biashara linalomilikiwa na wizara yetu”, ilikuwa inafaa kutoa nyaraka zinazohitajika.

4.1.2.5 Msumbiji

[48] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 175
[49] UNSC, S/2016/157, paragrafu ya 108
[50] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 182
[51] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 69
[52]UNSC, S/2016/157, paragrafu ya 94
[53] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 73

Jopo la Wataalamu lilipokea maelezo kuhusu usafiri baina ya 2012 na 2017 hadi na kutoka Msumbiji uliofanywa na raia watano wa Korea Kaskazini kwa niaba ya KOMID na Green Pine ambao walikuwa wamehusishwa na biashara ya silaha za kawaida na usafirishaji haramu wa silaha kwenye nchi zingine barani Afrika.[54] Raia wa Korea Kaskazini walisafiri hadi kwenye viwanja vya ndege vya kijeshi na kiraia vilivyoko mbali ambavyo vilkuwa na makao makuu ya jeshi karibu nazo.[55]

4.1.2.6 Zimbabwe

Jopo la Wataalamu linachunguza shughuli za raia wa Korea Kaskazini nchini ZImbabwe, ambao wana uhusiano na Green Pine na ambao wanahusishwa kwenye biashara ya silaha barani Afrika na kwenye Mashariki ya Kati.[56]

4.2 Glocom

4.2.1 Eritrea

Kampuni ya Eritech Computer Assembly & Comunications Technology PLC, ambayo inafanya shughuli zake chini ya mamlaka au uelekezi wa Vikosi vya Ulinzi cya Eritrea, ilituhumiwa kuwa ilikuwa inafanya kazi na Glocom wakati mzigo wa Eritech wa maboksi 45 ya bidhaa za kijeshi za mawasiliano ya redio, uliposhikwa.[57] Maboksi yalikuwa yamewekewa lebo ya “Glocom” na karibu bidhaa zote zilikuwa zimetangazwa na Glocom kwenye tovuti yake. Mzigo ulikuwa unatoka nchini Uchina.

5. Changamoto za Kutambua na Kuzuia Ukiukaji wa Vikwazo Vilivyowekewa Korea Kaskazini

Mifano ya ukiukaji wa vikwazo iliyofafanuliwa kwenye kifungu cha tatu inatambua hatua kadhaa ambazo zimetumiwa na mashirikisho ya Korea Kaskazini—na ambazo zina uwezekano mkubwa kuwa zitaendelea kutumiwa—ili kukwepa vikwazo.

5.1.1 Lakabu

Wawakilishi wa mashirikisho ya Korea Kaskazini mara nyingi huwa yanatumia lakabu ili kuficha utambulisho wao na ili kukwepa vikwazo vinvyowazuia wasisafiri kimataifa. Kwa mfano, Rais wa KOMID Kang Myong Chol mnamo 2013 na Rais wa Shirika Husiani la

[54] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 96

[55] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 76

[56] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 144

[57] UNSC, S/2017/150, paragrafu za 72-73

Green Pine Ri Hak Chol mnamo 2014 walisafiri hadi Irani kwa kutumia lakabu na pasipoti anuwai.[58]

Vivyo hivyo, mashirikisho yanatumia lakabu ili kuyaruhusu yaendelee kufanya shughuli ng'ambo bila kugunduliwa. Green Pine ni maarufu kuhusiana na haya, na kwa kutumia lakabu, wafanyakazi wake wamefungua ofisi kadhaa kwenye nchi zingine, ikiwemo nchini Irani na Uchina.[59]

5.1.2 Wanadiplomasia, wawakilishi, na mabalozi

Wawakilishi wa mashirikisho wanafanya shughuli zao kwenye balozi, wanashirikiana moja kwa moja na wanadiplomasia na wafanyakazi wa ubalozi, na wamepewa vyeti vya kuwa wanadiplomasia ili kurahisisha shughuli zao huko ng'ambo.

Kwa mfano, vyombo vya habari vimeripoti maafisa wa KOMID wanaofanya kazi kwenye balozi za Korea Kaskazini ili kurahisisha mauzo. Kulingana na gazeti la The New York Times, mwakilishi wa KOMID Son Jong Hyok alifanya kazi pamoja na Balozi Pak Chol Il wa Ubalozi wa Korea Kaskazini huko Kairo, Misri, ili kuuza silaha za Korea Kaskazini kwa nchi barani Afrika.[60] Ubalozi wenyewe ulifafanuliwa kuwa “pia unafanya shughuli kisiri kama biashara ya kieneo ya silaha” na “duka la silaha linalovuma la uuzaji kisiri wa makombora ya Korea Kaskazini na maunzi ya kijeshi ya zama za Kisovyeti kwa bei nafuu kwenye eneo la Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati”.

Jopo la Wataalamu pia liliona mfumo ambao Korea Kaskazini inawapatia wawakilishi wa ng'ambo wa Korea Kaskazini hadhi ya kidiplomasia.[61] Nchini Angola, kwa mfano, Kim Hyok Chan, mwanadiploamsia na mwakilishi wa Green Pine, alifanya mikataba, alitafuta na kununua vipuri, na alisimamia uundaji upya wa voti za wanamaji za kushika doria za Angola.[62] Mfano wa Kim Hyok Chan hauko pweke. Kuna ushahidi kuwa mwanadiplomasia wa pili, Jol Chol Young, pia alifanya shughuli kwa niaba ya Green Pine.[63]

5.1.3 Mipango ya usafiri

Ili kuficha safari zao na kule wanakoenda, wawakilishi wa Korea Kaskazini wanapitia nchi kadhaa, kwa mfano Uchina, Uhabeshi, Irani, Muungano wa Falme za Kiarabu,

[58] UNSC, S/2019/171, paragrafu ya 72

[59] UNSC, S/2017/150, paragrafu za 167, 172, 173

[60] Ibid. Walsh, New York Times.

[61] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 25

[62] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 207

[63] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 208

Urusi,[64] na wamenunua nauli za ndege kwenye nchi zingine, zikiwemo Jamhuri ya Kiarabu ya Siria na Misri.[65] Maafisa na wawakilishi wa mashirikisho pia wanasafiri na pasipoti anuwai, ambayo inafanya utekelezaji wa vikwazo—kwa mujibu wa nambari za pasipoti zilizojumuishwa kwenye orodha za vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataif—uwe ngumu.[66]

5.1.4 Modeli za Mtawanyiko za Kampuni

Modeli za Mtawanyiko za Kampuni zinafafanua mashirikisho ya Korea Kaskazini, na zinaruhusu uanzilishaji wa mitandao inayosaidia kutenganish kampuni binafsi na wanaofaidika na kampuni hizo nchini Korea Kaskazini na wale ambao si raia wa Korea Kaskazini ambazo wanashirikiana na kampuni za Korea Kaskazini kwenye nchi zingine.[67] Kwa mfano, Mansudae, iliyozungumziwa hapo juu kuhusiana na KOMID, ilikuwa kwenye orodha ya zaidi ya kampuni kumi zenye uhusiano na uchunguzi wa Paneli wa Kundi la Kampuni la Malesia na Korea (MKP).[68] Jopo liligundua shirikisho la kampuni zilizoorodheshwa ambalo lilikuwa linajumuisha Mansudae, MKP, Ofisi ya Jumla ya Upelelezi, Shirika la Banki la Korea Kwangson, na zingine.

5.2 Matawi na kampuni zifichazo

Kwa kushirikiana na miundo ya biashara zilizotawanyika, kampuni zifichazo zinatumiwa kuficha kuhusika kwa kampuni za Korea Kaskazini. Kwa mfano, tawi la Misri la KOMID lilianzishwa kwa usaidizi amilifu wa Pak Chun Il, ambaye alikuwa Balozi wa Korea Kaskazini nchini Misri.[69] Vivyo hivyo, KOMID ilianzisha kampuni zifichazo nchini Uchina, kama vile Kampuni Mpya ya Biashara ya Teknolojia ya Beijinh,[70] huku Glocom inafanya shughuli kwa kutumia kampuni zifichzo nchini Malesia.

5.3 Nchi za kirafiki

Ukiukaji wa vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini unasaidiwa na serikali za kirafiki zinazotoa usaidizi wa moja kwa moja au kivingine au kupuuza shughuli za Korea

---

[64] UNSC, S/2017/150, majedwali ya 8, 10 na 11

[65] UNSC, S/2017/150, jedwali la 8

[66] Tazama, kwa mfano, simtofahamu baina ya nambari za pasipoti za Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini Ri Won Ho kama zilizvoorodheshwa na Orodha Jumuishi ya Vikwazo na kwenye Ripoti ya S/2017/150. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Orodha Jumuishi ya Vikwazo vya Umoja wa Mataifa. UNSC, S/2017/150, Jedwali la 8.

[67] UNSC, S/2018/171, paragrafu ya 161

[68] UNSC, S/2017/742, paragrafu ya 57

[69] Gazeti la AlYoum AlJaded (Balozi wa Korea Kaskazini huko Kairo anakumbana na tishio la kufukuzwa nchini kwa ajili ya usafirishaji haramu wa silaha) 22 Machi, 2016

[70] UNSC, S/2017/150, paragrafu ya 163

Kaskazini. Kimahususi, Misri imechukuliwa kuwa ni rafiki wa karibu wa Korea Kaskazini, na haijaficha kuwa inaipatia usaidizi Korea Kaskazini.[71] Maafisa wa KOMID wamekuwa wakifanya shughuli zao nchini Irano na Shirikisho la Urusi.[72] Usafirishaji wa bidhaa zisizoruhusiwa kufanyiwa biashara pia zilikuwa zinatoka nchini Uchina.[73]

4.7 Kutumia wageni

Kuna mifano ambapo wageni maalum wanaisaidia Korea Kaskazini kukwepa vikwazo bila ya kuungwa mkono na nchi zao. Mfano mmoja maarufu ni ule wa raia wa Austria Josef Schwartz, ambaye, kupitia kampuni yake, Schwartz Motorbootservice & Handel GmbH, alisafirisha vifaa vya boti za kijeshi za kushika doria hadi nchini Angola.[74]

6. MAPENDEKEZO

6.1 Angalia kwa makini mipango na hati za usafiri

Kama ilivyofafanuliwa kwenye kifungu cha 5.3, kumekuwa na matukio ya maafisa wa Korea Kaskazini wakisafiri na zaidi ya pasipoti moja kwa niaba ya mashirikisho. Kwa hivyo, nambari za pasipoti zilizoorodheshwa kwenye orodha ya vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa zinaweza kuwa si zile ambazo zoinatumiwa na afisa anapokuwa anasafiri. Kwa hivyo ni muhimu kuangalia kwa makini hati za usafiri ili kuwatambua raia wa Korea Kaskazini waliopigwa marufuku wasisafiri kimataifa. Njia tata zisizo za kawaida za usafiri (kimahususi kwa kupitia nchi za kirafiki kama vile Irani, Siria, na Uchina) zinaweza kutumiwa kama kiashiria cha kutambua watu binafsi waliopigwa marufuku wasisafiri kimataifa.

6.2 Chunguza uhusiano na kampuni zingine

Mikakati ya miundo ya biashara zilizotawanyika, matawi na kampuni zifichazo, na kuingiza kampuni ndani ya mashirika ya nchi zingine, inatilia mkazo umuhimu wa kuchunguza uhusiano na kampuni zingine. Inapendekezwa makini idumishwe kwenye Orodha ya Umoja wa Mataifa ya Watu Binafsi, Kampuni, na Mashirika Yanayolengwa ili kung'amua kama kuna uhuisano baina ya kampuni na shirika lililolengwa. Hii ni muhimu haswa kwa ajili baadhi ya wahusika wa Korea Kaskazini wamekuwa wanajizatiti zaidi kuendelea na shughuli zao licha ya kuwa wameorodheshwa na Umoja wa Mataifa. Hii

[71] Donia Alwatan, https://www.alwatanvoice.com/arabic/news/2016/01/18/852255.html. 18 Jan 2016.

[72] UNSC, S/2016/157, Jedwali la 8 na pragrafu ya 175.

[73] UNSC, S/2017/150

[74] UNSC, S/2016/157, paragrafu ya 108

ndiyo hali ya Glocom, ambayo, kuanzia 2018, ili kuendelea kutangaza bidhaa zake kwenye vyombo vya kijamii.[75]

6.3 Jihadhari na Fursa za Bidhaa za Kijeshi, Usaidizi Husika, Huduma za Ujenzi

Ili kutekeleza uangalifu unaoeleweka na kampuni ambazo huenda zina uhusiano na Korea Kaskazini, ni muhimu kuwa makini kuhusu watu binafsi na mashirika ambayo yanajitolea kuuza bidhaa za kijeshi, usaidizi husika, au huduma za ujenzi. Upungufu wa uangalifu unaoeleweka wenye kubainisha unakuja na hatari madhubuti ya kuhusishwa na mradi wa silaha za nyuklia za Korea Kaskazini, wahusika wengine wakaidi kama vile Irani, na tishio ambalo, nchi hizo, kwa pamoja, zinasababisha kwa usalama wa kimataifa.

6.4 Boresha kuripoti kuhusiana na utiifu wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini

Mikakati anuwai inayotumiwa na mashirikisho ili kukwepa vikwazo inategemea usiri na ulaghai. Labda mojawapo kati ya njia zenye ufanisi zaidi za kupunguza ufanisi wa mikakati yao ni kuongeza kuripoti shughuli zinazoshukiwa za Korea Kaskazini kwa Umoja wa Mataifa. Uwazi zaidi unairuhusu Umoja wa Mataifa itoe maelezo bora kwa nchi wanachama, na unaweza kusaidia kutambua juhudi za Korea Kaskazini za kukiuka vikwazo.

Kuhusu Kathrin Kranz

Kathrin Kranz ana Ph.D. ya Mafunzo ya Amani na Sayansi ya Kisiasa kutoka Chuo Kikuu cha Notre Dame, na LL.M. ya Sheria ya Kimataifa ya Umma kutoka Shule ya Uchumi na Sayansi ya Kisiasa ya London. Utafiti wake unaangazia biashara ya kimataifa ya silaha, vikwazo vya uchumi, na taasisi za kimataifa.

[75] France 24 “Iliyodhihirishwa na Umoja wa Mataifa, kampuni ifichayo ya Korea Kaskazini inajificha hadharani,” 08.06.2018

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com